

KUMB: PPR/17 - 12/1

TAARIFA KWA UMMA KUHUSU BEI KIKOMO ZA MAFUTA AINA YA PETROLI KUANZIA JUMATANO, TAREHE 6 DECEMBER 2017

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), inatangaza bei kikomo za bidhaa za mafuta ya petroli hapa nchini. Bei hizi zitaanza kutumika kuanzia **Jumatano, Tarehe 6 Disemba 2017**. Pamoja na kutambua bei kikomo za bidhaa mbalimbali za petroli nchi nzima, ni muhimu kuzingatia yafuatayo:-

- (a) Bei za jumla na rejareja kwa mafuta ya aina zote yaani Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa zimeongezeka ikilinganishwa na toleo lililopita la tarehe 1 Novemba 2017. Kwa mwezi Disemba 2017, bei za rejareja za Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa zimeongezeka kwa Shilingi 41/lita (sawa na asilimia 1.96), Shilingi 30/lita (sawa na asilimia 1.54) na Shilingi 3/lita (sawa na asilimia 0.17) sawia. Vilevile, kwa kulinganisha na toleo la mwezi uliopita, bei za jumla za Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa zimeongezeka kwa Shilingi 41.42/lita (sawa na asilimia 2.06), Shilingi 30.01/lita (sawa na asilimia 1.63) na Shilingi 3.27/lita (sawa na asilimia 0.18) sawia. Ongezeko la bei za mafuta ya Dizeli na Mafuta ya Taa limetokana na ongezeko la ghamama za usafirishaji (*BPS Premiums*) na ongezeko la bei za mafuta hayo katika soko la dunia, wakati, ongezeko la bei ya mafuta ya Petroli limetokana na ongezeko la ghamama za kusafirisha mafuta hayo. Kumekuwa na ongezeko la bei kwa mafuta yote (Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa), japokuwa kumekuwa na kuimarika kwa Shilingi ya Tanzania dhidi ya Dola ya Marekani, fedha inayotumika kununulia mafuta.
- (b) Bei za jumla na rejareja kwa mafuta ya Petroli na Dizeli katika mkoa wa Tanga nazo zimeongezeka ikilinganishwa na toleo lililopita la tarehe 1 Novemba 2017. Bei za Mafuta ya Taa hazijabadilika kwa sababu hakuna Mafuta ya Taa yaliyopokelewa katika bandari ya Tanga katika mwezi wa Novemba 2017. Katika toleo hili, bei za rejareja za Petroli kwa Mikoa ya Kaskazini zimeongezeka kwa Shilingi 43/lita (sawa na asilimia 2.02) wakati bei za Dizeli zimepungua kwa Shilingi 9/lita (sawa na asilimia 0.45). Aidha, kwa kulinganisha na toleo la mwezi uliopita, bei za jumla za Petroli zimeongezeka kwa Shilingi 42.52/lita (sawa na asilimia 2.13) wakati bei za Dizeli zimepungua kwa Shilingi 9.08/lita (sawa na asilimia 0.48). Mabadiliko ya bei za mafuta ya Petroli na Dizeli katika mkoa wa Tanga yanatokana na kuongezeka kwa ghamama za usafirishaji (*BPS premiums*) na mabadiliko ya bei za mafuta hayo katika soko la dunia japokuwa kumekuwa na ongezeko la thamani ya Shilingi ya Tanzania dhidi ya Dola ya Marekani, fedha inayotumika kununulia mafuta.
- (c) Mamlaka inapenda kuukumbusha umma kwamba bei kikomo za mafuta kwa eneo husika, zinapatikana pia kupitia simu za mkononi kwa kupiga namba ***152*00#** na kisha kufuata maelekezo. Huduma hii ni bure na inapatikana kupitia mitandao yote ya simu za mkononi hapa nchini.
- (d) Kwa mujibu wa Sheria ya Mafuta ya mwaka 2015, bei za bidhaa za mafuta ya petroli zitaendelea kupangwa na soko. EWURA itaendelea kuhamasisha ushindani kwa kutoa taarifa za bei kikomo za bidhaa za mafuta. Taarifa hizi zina lengo la kuwasaidia wadau kufanya maamuzi stahiki kuhusu manunuzi ya bidhaa za mafuta.

- (e) **Kampuni za mafuta ziko huru kuuza bidhaa za mafuta ya petroli kwa bei ya ushindani mradi tu bei hizo zisivuke bei kikomo (price cap)** kama ilivyokokotolewa na kanuni (*formula*) iliyopitishwa na EWURA na ambayo ilichapishwa katika **Gazeti la Serikali Na. 216/2017 la mwezi Mei 2017.**
- (f) Vituo vyote vya mafuta vinatakiwa kuchapisha bei za bidhaa za mafuta katika mabango yanayoonekana bayana na yakionesha bei ya mafuta, punguzo, vivutio vya biashara au promosheni zinazotolewa na kituo husika. Pale ambapo inawezekana kuchagua, wateja wanashauriwa kununua bidhaa za mafuta katika vituo vinavyouza mafuta kwa bei nafuu zaidi ili kushamirisha ushindani. **Ni kosa kuuza mafuta bila kuweka mabango ya bei inayoonekana vizuri kwa wateja. Adhabu kali itatolewa kwa kituo husika kwa kutotekeleza matakwa ya kisheria kwa mujibu wa kanuni husika.**
- (g) Wauzaji wa mafuta ya petroli wanatakiwa kutoa risiti za mauzo kutoka kwenye mashine za EFPP (*Electronic Fiscal Pump Printers*) na Wanunuzi wahakikishe wanapata stakabadhi hizo za malipo zinazoonyesha jina la kituo, tarehe, aina ya mafuta yaliyonunuliwa na bei kwa lita. Stakabadhi hizo za malipo zitatumika kama kidhibiti cha wanunuzi wa mafuta endapo kutajitozea malalamiko ya aidha kuuziwa mafuta kwa bei ya juu kuliko bei kikomo au kuuziwa mafuta yasiyo na kiwango cha ubora kinachofaa, na pia, risiti hizo zitasaidia kurahishisha ukusanyaji wa kodi za Serikali zitokanazo na mafuta ya petroli.

A: BEI ZA REJAREJA

Mji	Bei Kikomo		
	Petroli (Shs/Lita)	Dizeli (Shs/Lita)	Mafuta Ya Taa (Shs/Lita)
Dar es Salaam	2,160	1,984	1,942
Arusha	2,203	2,046	1,995
Arumeru (Usa West)	2,203	2,046	1,995
Karatu	2,222	2,065	2,013
Monduli	2,209	2,052	2,000
Monduli-Makuyuni	2,213	2,056	2,005
Ngorongoro (Loliondo)	2,288	2,131	2,079
Kibaha	2,164	1,989	1,947
Bagamoyo	2,171	1,995	1,953
Kisarawe	2,167	1,991	1,949
Mkuranga	2,170	1,994	1,952
Rufiji	2,187	2,012	1,970
Dodoma	2,218	2,043	2,001
Bahi	2,226	2,050	2,008
Chemba	2,245	2,069	2,027
Kondoa	2,251	2,076	2,034
Kongwa	2,216	2,040	1,998
Mpwapwa	2,220	2,044	2,002
Iringa	2,224	2,048	2,006
Kilolo	2,228	2,053	2,011
Mufindi (Mafinga)	2,234	2,058	2,016

Njombe	2,252	2,076	2,034
Ludewa	2,290	2,114	2,072
Makete	2,283	2,107	2,065
Wanging'ombe (Igwachanya)	2,250	2,074	2,032
Bukoba	2,375	2,199	2,157
Biharamulo	2,349	2,173	2,132
Karagwe (Kayanga)	2,391	2,215	2,174
Kyerwa (Ruberwa)	2,397	2,221	2,179
Muleba	2,375	2,199	2,157
Ngara	2,340	2,165	2,123
Misenyi	2,383	2,208	2,166
Geita	2,325	2,149	2,107
Bukombe	2,314	2,138	2,096
Chato	2,346	2,170	2,128
Mbogwe	2,363	2,187	2,145
Nyang'hwale	2,340	2,164	2,122
Kigoma	2,391	2,215	2,173
Uvinza (Lugufu)	2,403	2,227	2,185
Buhigwe	2,380	2,204	2,162
Kakonko	2,348	2,172	2,130
Kasulu	2,377	2,201	2,159
Kibondo	2,355	2,179	2,137
Moshi	2,193	2,036	1,984
Hai (Bomang'ombe)	2,196	2,039	1,988
Mwanga	2,186	2,029	1,977
Rombo (Mkuu)	2,210	2,053	2,001
Same	2,179	2,022	1,971
Siha (Sanya Juu)	2,199	2,043	1,991
Lindi	2,219	2,043	2,001
Lindi-Mtama	2,237	2,061	2,019
Kilwa Masoko	2,194	2,018	1,976
Liwale	2,240	2,064	2,022
Nachingwea	2,248	2,072	2,030
Ruangwa	2,249	2,074	2,032
Babati	2,237	2,080	2,029
Hanang (Katesh)	2,248	2,091	2,039
Kiteto (Kibaya)	2,252	2,096	2,044
Mbulu	2,250	2,093	2,041
Simanjiro (Orkasumet)	2,269	2,112	2,061
Musoma	2,338	2,162	2,120
Musoma Vijijini (Busekela)	2,379	2,203	2,161
Rorya (Ingirijuu)	2,347	2,171	2,129
Rorya (Shirati)	2,382	2,206	2,164
Bunda	2,329	2,153	2,112
Butiama	2,335	2,159	2,117
Serengeti (Mugumu)	2,384	2,208	2,166
Tarime	2,349	2,173	2,131
Tarime (Kewanja/Nyamongo)	2,354	2,178	2,136

Mbeya	2,267	2,091	2,049
Chunya	2,276	2,101	2,059
Chunya (Makongolosi)	2,290	2,115	2,073
Ileje	2,280	2,104	2,062
Kyela	2,282	2,107	2,065
Mbarali (Rujewa)	2,251	2,075	2,033
Mbozi (Vwawa)	2,276	2,100	2,058
Momba (Chitete)	2,285	2,109	2,067
Rungwe (Tukuyu)	2,276	2,100	2,058
Morogoro	2,185	2,009	1,967
Mikumi	2,200	2,025	1,983
Kilombero (Ifakara)	2,223	2,047	2,005
Kilombero (Mlimba)	2,245	2,069	2,027
Kilombero (Mngeta)	2,234	2,058	2,017
Ulanga (Mahenge)	2,233	2,058	2,016
Malinyi	2,243	2,068	2,026
Kilosa	2,203	2,028	1,986
Gairo	2,203	2,028	1,986
Mvomero (Wami Sokoine)	2,195	2,020	1,978
Turiani	2,210	2,034	1,992
Mtwara	2,232	2,056	2,015
Nanyumbu (Mangaka)	2,281	2,105	2,063
Masasi	2,258	2,082	2,040
Newala	2,264	2,088	2,047
Tandahimba	2,257	2,082	2,040
Mwanza	2,310	2,134	2,092
Kwimba	2,346	2,170	2,128
Magu	2,318	2,142	2,100
Misungwi	2,315	2,140	2,098
Sengerema	2,342	2,166	2,124
Ukerewe	2,369	2,193	2,151
Sumbawanga	2,332	2,157	2,115
Kalambo (Matai)	2,340	2,164	2,122
Nkasi (Namanyele)	2,346	2,170	2,128
Katavi (Mpanda)	2,367	2,192	2,150
Mlele (Inyonga)	2,346	2,170	2,128
Songea	2,283	2,107	2,065
Mbinga	2,316	2,141	2,099
Namtumbo	2,312	2,137	2,095
Nyasa (Mbamba Bay)	2,319	2,143	2,101
Tunduru	2,342	2,166	2,124
Shinyanga	2,288	2,113	2,071
Kahama	2,302	2,126	2,084
Kishapu	2,317	2,141	2,099
Simiyu (Bariadi)	2,330	2,154	2,112
Busega (Nyashimo)	2,323	2,147	2,105
Itilima (Lagangabilili)	2,333	2,157	2,115
Maswa	2,321	2,146	2,104

Meatu (Mwanhuzi)	2,328	2,153	2,111
Singida	2,250	2,075	2,033
Iramba	2,262	2,087	2,045
Manyoni	2,235	2,059	2,017
Ikungi	2,246	2,070	2,028
Mkalama (Nduguti)	2,275	2,099	2,057
Tabora	2,314	2,138	2,096
Igunga	2,268	2,092	2,050
Kaliua	2,332	2,156	2,114
Ulyankulu	2,326	2,150	2,108
Nzega	2,278	2,103	2,061
Sikonge	2,325	2,150	2,108
Urambo	2,327	2,151	2,109
Tanga	2,147	1,990	1,938
Handeni	2,167	2,010	1,959
Kilindi	2,182	2,025	1,974
Korogwe	2,159	2,002	1,950
Lushoto	2,168	2,011	1,960
Mkinga (Maramba)	2,154	1,997	1,945
Muheza	2,152	1,995	1,943
Pangani	2,153	1,997	1,945

B: BEI ZA JUMLA

Bei za Jumla – DSM	Petroli (Shs/Lita)	Dizeli (Shs/Lita)	Mafuta ya Taa (Shs/Lita)
Bei Kikomo	2,048.86	1,873.15	1,831.27

Bei za Jumla - TANGA	Petroli (Shs/Lita)	Dizeli (Shs/Lita)	Mafuta ya Taa (Shs/Lita)
Bei Kikomo	2,035.78	1,878.92	1,827.17

Mhandisi Godwin Samwel
KAIMU MKURUGENZI MKUU
EWURA